JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 09 - 2019/2020**

**DHIDI YA**

**SAM MISAGO TV**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**

## 1.0 Utangulizi

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa huduma za utangazaji kwa **SAM MISAGO TV**, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mitandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mitandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yo yote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

1.3 Tarehe 07 Februari, 2020, **SAM MISAGO TV** ilichapisha/kuweka mtandaoni kupitia chaneli yake ya YouTube maudhui yenye lugha za matusi na yenye kushabikia vitendo vya ngono.

1.4 **SAM MISAGO TV** ilichapisha na kutangaza maudhui hayo bila ya kuzingatia Weledi, Sheria, Kanuni na Maadili ya uandishi wa habari kwa sababu mmiliki/mhariri wa chaneli hiyo aliweka/alichapisha picha jongefu iliyomuonesha msanii wa muziki aitwaye **Amber Lulu** akiwa anacheza muziki wakati ameinamisha kiuno na mtu mwingine akiwa upande wake wa nyuma akimchezea kwa viashiria vya kufanya ngono.

1.5 Vile vile, **SAM MISAGO TV** ilichapisha/kuweka mtandaoni kupitia chaneli yake ya Youtube maudhui yenye lugha ya matusi katika picha jongefu yenye kichwa cha habari ***Kimenuka, Hasira, Matusi, kutoka kwa Jacqueline Wolper, Msichukulie poa Nimepanic*** ambapo msanii wa

filamu aitwaye **Jacquline Wolper** alikuwa akihojiwa na mtangazaji wa chaneli hiyo.

1.6 Katika picha jongefu hiyo, **Bi. Jacqueline Wolper** alisikika akizungumza maneno yafuatayo,***...Usiseme kwamba unammudu mtu, halafu unaenda unaitwa, unapewa kitita cha hela labda sijui milioni tano sijui milioni kumi halafu eti unasema oya Wolper huyu mshikaji wangu huyu mtu wangu tumsaidie, fuck!.***

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kitendo cha kuweka maudhui yenye lugha ya matusi na yenye kushabikia vitendo vya ngono, **SAM MISAGO TV** inatuhumiwa kukiuka Kanuni Na. 5(1) (a), (b), 5 (2) (b), 12 (a), (b), (d), (e), (h), and (k) (i) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni) 2018, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo;-

*5.-(1) For the purpose of these Regulations, an online content provider shall have the obligations to-*

*(a) ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law;*

*(b) take into account trends and cultural sensitivities of the general public;*

*5.- (2) A subscriber and user of online content services shall:*

*(b) ensure his posts do not contravene the provision of these Regulations and any other written law.*

*12. Online content services provider shall not publish-*

*(a) indecent content saves for sex and nudity sex scenes approved by the body responsible for film censorship;*
*(b) obscene content;*
*(d) explicit sex acts or pornography;*
*(e) sex crimes, rape or attempted rape and statutory rape, or bestiality;*
*(h) content that causes annoyance, threatens harm or evil, encourages or incites crime, or leads to public disorder;*
*(k) content that uses bad language including-*

*(i) the use of disparaging or abusive words which is calculated to offend an individual or a group of persons.*

## 3.0 Wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maudhui

Tarehe 03 Machi, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia Uongozi wa **SAM MISAGO TV,** wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 11 Machi, 2020, saa 04:00 asubuhi, uongozi wa **SAM MISAGO TV** ukiwakilishwa na Bw. Faudhi Jafari, Meneja wa Maudhui na Mwandishi wa Habari, ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

## 4.0 Kusomewa Shitaka na Kuangalia Maudhui ya SAM MISAGO TV

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **SAM MISAGO TV** shitaka lao. Pia, Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **SAM MISAGO TV** walisikiliza na kuangalia maudhui mtandaoni yaliyochapishwa na kutangazwa na **SAM MISAGO TV**, tarehe 07 Februari, 2020 na kisha kuutaka Uongozi huo kujitetea ni kwanini wasichukuliwe hatua za kisheria dhidi ya tuhuma za kukiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni.

## 5.0 Maelezo ya Utetezi ya SAM MISAGO TV

Katika utetezi wao wa maandishi, Uongozi wa **SAM MISAGO TV** umeanza kwa kukiri kosa na kuomba radhi kwa kuvunja Sheria na masharti ya leseni kwa kuchapisha mtandaoni kupitia chaneli yao ya YouTube, maudhui ambayo hayakupitiwa na kukaguliwa vizuri. Wamesema kuwa hatua zimeshachukuliwa za kurekebisha makosa hayo kwa kufuta maudhui hayo mtandaoni, na pia kuhakikisha kuwa maudhui yao yanakaguliwa na watu wawili kabla hawajayachapisha mtandaoni. Wamemalizia kwa kuahidi kutorudia tena kosa hilo.

Pamoja na utetezi wao wa maandishi, **SAM MISAGO TV** waliendelea kueleza yafuatayo:-

5.1 **Bw. Faudhi Jafari**, Meneja wa Maudhui na Mwandishi wa Habari, aliomba radhi kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kusimamia maudhui hayo kabla hayajachapishwa. Alidai kuwa maudhui yanayolalamikiwa yalichapishwa na wanafunzi ambao walikuwa wakifanya mafunzo kwa vitendo katika Kituo chao. Alisema kuwa wamefanya semina kwa wafanyakazi wao na kwamba wamelielewa kosa.

## 6.0 Majumuisho ya Utetezi wa SAM MISAGO TV

Katika kujumuisha utetezi wao, **Bw. Faudhi Jafari** aliiomba Kamati iwasamehe kwa kuwa hili ni kosa lao la kwanza na kuahidi kutolirudia kosa hilo.

## 7.0 Tathmini ya Kamati

7.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **SAM MISAGO TV** imefanya kosa la kuchapisha na kutangaza, maudhui yenye lugha ya matusi na yanayohamasisha/kushabikia vitendo vya ngono kinyume na Kanuni Na. 5(1) (a), (b), 5 (2) (b), 12 (a), (b), (d), (e), (h), na (k) (i) za Kanuni za

Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni) 2018; na kama ambavyo wamekiri wenyewe.

7.2 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa **SAM MISAGO TV** kuwa maudhui hayo yalichapishwa na wanafunzi ambao walikuwa wakifanya mafunzo kwa vitendo kituoni hapo hauna mashiko kwa sababu wanatakiwa kuimarisha usimamizi na uhariri wa maudhui yao ili kuhakikisha wafanyakazi na wanafunzi wao wanachapisha maudhui bora yanayozingatia Sheria, Kanuni, Taaluma, Weledi na Maadili ya uandishi wa habari;

7.3 Kamati ya Maudhui imeona kuwa **SAM MISAGO TV** imeshindwa kutumia kwa vizuri dhamana kubwa ambayo Serikali imevipa vyombo vya utangazaji ya kuhakikisha kwamba vinaimarisha ustawi wa jamii na Taifa.;

## 8.0 Ushauri wa Kamati kwa SAM MISAGO TV

Kamati ina lengo la kuimarisha tasnia ya habari na utangazaji na kuwa haina nia ya kubana ubunifu wa watangazaji, bali inawataka wanahabari kuzingatia weledi, Sheria, Kanuni na maadili.

Hata hivyo, kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **SAM MISAGO TV** yafuatayo:-

8.1 Kuimarisha Usimamizi na Uhariri wa maudhui yao kabla ya kuyachapisha mtandaoni kupitia chaneli yao ili kuhakikisha maudhui yanayochapishwa ni salama;

8.2 Kuweka utaratibu wa kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara wafanyakazi na wanafunzi wao ili kuwajengea uwezo waweze kuzingatia Weledi, Sheria, Kanuni, Maadili, na Taaluma katika kazi zao.

## 9.0 Uamuzi wa Kamati

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **SAM MISAGO TV**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **SAM MISAGO TV** kupitia chaneli yake mtandaoni ya YouTube imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018 kwa kuchapisha maudhui yenye lugha ya matusi na yanayohamasisha vitendo vya ngono.

Hivyo, Kamati ya Maudhui inaamua kutoa adhabu zifuatazo kwa **SAM MISAGO TV**;

1. Kulipa faini ya Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00) tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mujibu wa Kanuni Na. 18 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018;

2. Kupewa Onyo;

3. Kuomba radhi kwa watazamaji na wasikilizaji wao kupitia chaneli yao ya YouTube iliyotumika kutendea kosa hili, kwa siku saba (7) mfululizo kuanzia tarehe 18 Machi, 2020.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo **17 Machi, 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bwana Joseph Method Mapunda**

...............................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI WAFUATAO:**

**1. Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**..........................................

**2. Bwana Derek Kaitira Murusuri**...........................................

**3. Bwana Jacob Gregory Tesha**...........................................